**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

**MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA**

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

# MAELEZO YA MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA (TMDA) – DKT. ADAM M. FIMBO, WAKATI WA UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA WAHARIRI NA WAANDISHI WA HABARI UKUMBI WA HOTELI YA SUNSET IRINGA TAREHE 16 - 17 MEI, 2024

- **Mkuu wa Mkoa wa Iringa,**
- **Mganga Mkuu wa Mkoa,**
- **Wakurugenzi na Watumishi wa TMDA,**
- **Wanahabari,**
- **Wageni waalikwa,**
- **Mabibi na Mabwana.**

Awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kuwakaribisha wote kwenye kikao kazi hiki muhimu cha Wahariri na Waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari vilivyoko katika mikoa ya Dodoma, Singida na Iringa.

Aidha, nawiwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako Mgeni Rasmi Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Mhe. Peter Serukamba kwa kukubali kuja kufungua kikao kazi hiki licha ya majukumu mengine mengi na muhimu ya kitaifa uliyonayo.

Kwa namna ya pekee, pia niwashukuru Wahariri na Waandishi wa habari kwa kuitikia mwaliko wetu na kuhudhuria mafunzo haya. Hii inaonyesha dhamira njema mliyonayo na utayari wa kushirikiana na TMDA katika kutimiza lengo lake kuu la kulinda afya ya jamii kwa kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

**Mhe. Mgeni Rasmi,**

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ni taasisi ya Serikali iliyoanzishwa chini ya kifungu Na. 4(1) cha Sheria Na. 1, ya Dawa na Vifaa Tiba Sura 219 iliyoanza kutumika rasmi tarehe 1 Julai, 2003 pamoja na marekebisho yake kupitia Sheria ya Fedha Na. 8 ya mwaka 2019.

Kwa mujibu wa Sheria, TMDA imeanzishwa ili kuimarisha udhibiti wa usalama, ubora na ufanisi wa bidhaa za dawa, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa zinazohusiana na afya hapa nchini. lengo mahususi la kuhakikisha kwamba zipo salama, zina ubora na ufanisi unaokubalika ndizo zinazosambazwa na kutumika hapa nchini.

**Mhe. Mgeni Rasmi,**

Katika kipindi chote cha miongo miwili toka kuanzishwa kwa TMDA imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kufikia malengo yake kwa kuhakikisha kwamba jamii inakuwa salama kutokana na matumizi ya dawa, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyinginezo zinazohusiana na afya.

Mamlaka imefanikiwa kuweka na kuimarisha mifumo ya udhibiti wa bidhaa hapa nchini ikiwemo mifumo ya tathmini na usajili wa bidhaa, ukaguzi wa viwanda na maeneo ya biashara, utoaji na uingizaji bidhaa, ufuatiliaji wa usalama wa dawa pamoja na majaribio ya dawa.

Maboresho ya mifumo yameifanya Mamlaka kufikia na kushikilia Ngazi ya tatu ya Shirika la Afya Duniani – WHO (WHO Maturity L-3) kati ya nne kwa kuwa na mifumo bora ya udhibiti wa dawa hivyo kuwa taasisi ya kwanza ya udhibiti barani Afrika kufikia ngazi hiyo mwaka 2018. Aidha mifumo ya utendaji kazi na utoaji huduma imepata ithibati kwa kiwango cha kimataifa cha ISO 1901:2015 na ile ya maabara ISO/IEC 17025:2007

**Mhe. Mgeni Rasmi,**

TMDA katika utekelezaji wa majukumu yake inafanya chunguzi za kiimabara ili kufanya maamuzi ya kisayansi katika kujiridhisha ubora, usalama na ufanisi wa

bidhaa. Mamlaka imewekeza vya kutosha katika maabara kwa kuweka vifaa vya kisasa na mafunzo ya wataalamu. Uwekezaji huu umeifanya maabara ya TMDA kuwa maabara inayoaminiwa na kutumika kama maabara rejea barani Afrika. Pia, maabara ya dawa imepata ithibati na hivi karibuni maabara ya upimaji wa vifaa tiba na vitendanishi imepata ithibati katika njia 12 za kiuchunguzi. Hii ni hatua kubwa katika kuhakikisha usalam wa afya za wananchi kwa kuwa matokeo ya udhibiti yanakubalika duniani na kuondoa hofu katika ubora. Kupitia kikao hiki naomba kuwaalika watu binafsi, watafiti, na wazalishaji kuitumia maabara ya TMDA kwa ajili ya huduma za kiuchunguzi kwa bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi kutoka viwandani.

**Mhe. Mgeni Rasmi,**

Mamlaka inaendelea kuboresha huduma zake kwa kuzingatia maoni ya wateja pamoja na matumizi ya TEHAMA katika kutoa huduma ambapo kwa sasa huduma zote za Mamlaka zinatolewa kwa njia ya mtandao kitu ambacho kimeharakisha utoaji huduma na kupunguza gharama na usumbufu kwa wateja. Aidha, suala la utoaji wa elimu kwa makundi mbalimbali ya wananchi na wadau limepewa kipaumbele katika kuhakiksha kuwa walaji/watumiaji wa bidhaa zinazosimamiwa na Mamlaka wana taarifa sahihi kuhusu ubora usalama na ufanisi wake.

**Mhe. Mgeni Rasmi,**

Pamoja ni jitahada za Mamlaka katika kutoa elimu kwa jamii ili bado uelewa wa wananchi na wadau kuhusu shughuli za udhibiti zinazofanywa na Mamlaka uko chini kitu kinachoathiri utendaji wa Mamlaka. Kiwango hiki cha uelewa kimesababisha matumizi yasiyo sahihi ya dawa, idadi ndogo ya wananchi wanaoripoti maudhi ya dawa, baadhi ya wafanyabiashara kuingiza dawa duni na bandia pamoja na wananchi kutozingatia tarehe ya kuisha matumizi ya bidhaa.

Hali hii inapelekea Mamlaka kuendelea kutumia mbinu mbalimbali kuelimisha jamii. Mamlaka inatambua mchango wa vyombo vya habari katika kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu shughuli za udhibiti zinazofanywa na Mamlaka na kwamba uelewa mzuri wa waandishi na wahariri wa vyombo vya habari ni msingi wa uelimishaji jamii. Hivyo kikao kazi hiki kimejikita katika kutambua mchango na kuwaongezea uelewa zaidi wadau hawa muhimu katika kuelimisha jamii.

Ni wazi kuwa Wahariri na Waandishi wa Habari wana nafasi kubwa katika kuhakikisha kuwa Mamlaka inajulikana kwa jamii na Sheria ya Dawa na Vifaa

Tiba, Sura, 2019 inasimamiwa kwa ufanisi. TMDA imekuwa na utaratibu wa kukutana na wadau hawa muhimu kwa lengo la kuwaelimisha juu ya kazi zake sanjari na kuwakumbusha wajibu wa kila mdau katika kutekeleza Sheria husika.

**Mhe. Mgeni Rasmi,**

Suala la uelimishaji jamii limepewa kipaumbele kikubwa na TMDA na ndiyo sababu tumewaita hapa Wahariri walioko mbele yako kwa lengo la kuwashirikisha na kuhamasisha kuhusu majukumu ya Mamlaka ili kujadiliana kwa pamoja namna ya kushirikiana katika kuhakikisha kuwa soko la Tanzania lina bidhaa zilizo bora, salama na fanisi ili kumlinda mlaji.

Kwa kipindi kirefu sasa toka kuanzishwa kwake Mamalaka imekua ikiwahusisha wanahabari katika kutekeleza majukumu yake ya kiudhibiti. Mathalani, katika shughuli za uteketezaji bidhaa, operesheni maalum, na katika kutoa elimu kwa umma Mamalaka imekuwa ikiwatumia waandishi wa habari kufikisha ujumbe kwa jamii. Hata hivyo katika kuwajengea uwezo vikao kazi vimekuwa vikifanyika ukichukumlia mfano wa miaka mitano nyuma, vikao vilifanyika katika mikoa mbalimbali.

Kwa mwaka 2019 ulifanyika Bagamoyo mkoani Pwani ambapo kikao kilifunguliwa na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMDA D.k.t Adam M. Fimbo, mwaka 2020 kikao kilifanyika mkoani Morogoro ambapo kilifunguliwa na Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Morogoro Bw.Anza Ndossa kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, kwa mwaka 2021 kikao kilifanyika mkoani Arusha na kufunguliwa na Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Bi. Vones Oisso.

Vilevile mwaka 2022 TMDA iliendesha kikao na wanahabari mkoani Mbeya kilichofunguliwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mhe. Juma Homera na mwaka 2023 mkoani Dar es salaam na kilifunguliwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam, Mhe. Amos Makala.

Kimsingi, kazi ya kuelimisha umma sio rahisi na inahitaji ushirikiano wa karibu kati yetu sisi TMDA, waandishi wa habari na wananchi wote kwa ujumla wao. Ni matumaini yetu kwamba kupitia tasnia ya habari, tutaweza kuwafikia wananchi wengi zaidi na kuwapa elimu endelevu ili waweze kufanya maamuzi sahihi wakati wa kuchagua, kununua na kutumia bidhaa zinazodhibitiwa na TMDA.

**Mhe. Mgeni Rasmi,**

Mamlaka kwa kutambua mchango wa Waandishi wa habari na kuleta hamasa katika kuelimisha jamii kuhusu masuala ya udhibiti wa dawa, vifaa tiba,vitendanishi na bidhaa za tumbaku kupitia vyombo vya habari imekuwa ikitoa tuzo maalum kwa Waandishi ambao wameripoti mara nyingi taarifa na kuandaa Makala mbalimbali kuhusu kazi na majukumu ya TMDA kwa mwaka husika. Katika kikao kazi hiki tuzo zitatolewa kwa washindi wane (4) baada ya zoezi la kushindanisha kazi za waandishi kufanyika. Tuzo hizi zinatolewa kwa mara ya tatu sasa toka kuanzishwa kwake mwaka 2021/22.

**Mhe. Mgeni Rasmi,**

Kikao kazi hiki kinafanyika kwa siku mbili kwa kuwakutanisha wahariri na waandishi wa habari kutoka mikoa ya Dodoma, Singida na Iringa ambapo katika siku ya kwanza, washiriki ni Wahariri wa Habari na siku ya pili ni Waandishi wa Habari.

**Mhe. Mgeni rasmi,**

Mada mbalimbali zitawasikishwa katika kikao hiki ambapo ni matarajio yetu kuwa baada ya semina hii, washiriki waweze kuelewa vyema sheria na majukumu ya TMDA ili tushirikiane katika kulinda afya ya jamii.

Aidha, kupitia hoja zitakazoibuliwa baada ya mada husika kutolewa, tutaainisha kwa pamoja maeneo ya ushirikiano katika kuielimisha zaidi jamii kupitia vyombo vya habari juu ya masuala mbalimbali yahusuyo udhibiti wa bidhaa za dawa vifaa tiba na vitendanishi kutokana na ukweli kwamba usimamizi wa Sheria hautakuwa na mafanikio kama hatutakuwepo na ushirikishwaji wa wadau wetu hususan vyombo vya habari.

Ni imani yetu kuwa Wahariri na Waandishi hawa wakirudi kwenye maeneo yao ya kazi wataweza kueneza ujumbe watakaopata leo kwa watu wengi zaidi na hivyo kuwezesha jamii kupata elimu, kujilinda na kutumia dawa, vifaa tiba na vitendanishi vilivyosajiliwa au kupitishwa na TMDA.

Baada ya kusema haya ninayo heshima ya kuomba kuwashukuru tena wote kwa kutenga muda wenu na kufika na mwisho lakini si kwa umuhimu, naomba nichukue fursa hii kumkaribisha **Mgeni Rasmi**, Mkuu wa Mkoa wa Iringa ili aweze kutufungulia kikao kazi hiki.

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza**

**Karibu sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Iringa**

---

**MWISHO**